

Maswali

1. Nani alikuwa anafundishwa kuwa kuhani kwa Hekalu ya Yerusalemu?
2. Mbona Ezekieli na watu walikuwa na uoga?
3. Nini ilifanyika kwa Ezekieli na kwa watu?
4. Huko Babeli walipelekwa kuishi wapi?
5. Mbona Ezekieli alikasirika zaidi?
6. Nini ilifanyika kwa Ezekieli alipotimia miaka 30?
7. Mungu alipea Ezekieli kazi gani?
8. Wayahudi walijuaje kwamba Ezekieli alizungumza ujumbe wa kweli kutoka kwa Mungu?
9. Ezekieli aliwapa watu ujumbe gani?
10. Mungu alilinda watu wake walipokuwa watumwa kule Babeli?

Majibu

1. Ezekieli alikuwa anafundishwa kuwa kuhani kwa Hekalu ya Yerusalemu.
2. Waliogopa kwa sababu Mfalme Nebukadreza na jeshi lake kubwa walikuwa wanakuja Yerusalemu kuwashambulia.
3. Ezekieli na watu wengine 10,000 walipelekwa Babeli kama watumwa.
4. Walipelekwa kuishi kando ya Mto wa Kaberi kaskazini mwa mji wa Babeli.
5. Kwa sababu Ezekieli hangeweza kutumikia Mungu kama kuhani.
6. Ezekieli aliona maono ya ajabu ya utukufu wa Mungu.
7. Mungu aliita Ezekieli kuwa nabii wa kuzungumza na watu.
8. Mungu alifanya Ezekieli bubu. Angezungumza tu ikiwa Mungu amempa ujumbe.
9. Yerusalemu ingeharibiwa. Wangeishi Babeli kwa miaka 70. Walitakiwa wakubali ujumbe wa Mungu na watulie Babeli.
10. Ndiyo. Popote walipo watu wa Mungu, Mungu ako hapo na anawalinda.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



80 Nabii Ezekieli

Kwa Biblia

Ezekieli 1:1—4; Ezekieli 2: 1—5; Ezekieli 3: 26—27


Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu analinda watu wake mahali popote walipo. Mungu alitumia watu ujumbe kupitia kwa nabii Ezekieli

Somo

Ezekieli aliishi Yerusalemu. Alizaliwa kwa familia ya manabii. Ezekieli alikuwa anajifunza kuwa kuhani huko Yerusalemu. Makuhani huanza huduma huu wanapofika umri wa miaka 30. Ezekieli aliishi wakati wa hatari. Kwa muda wa miaka saba, Nebukadreza, Mfalme wa Babeli alikuwa ameshambulia na kuingia nchi ya Israeli. Alikuwa amechukua watu wengi kama wafungwa kutoka Yerusalemu mpaka Babeli. Danieli pamoja na marafiki wake watatu, wakuu wengi nao walichukuliwa kwenda Babeli.

Ezekieli na watu wa Yerusalemu waliogopa sana. Walisikia kwamba jeshi kubwa la Mfalme Nebukadreza lilikuwa linakuja kushambulia Yerusalemu tena. Wote walikumbuka wakati wenye Nabukadreza alikuja, akachukua watu wao mateka mpaka Babeli. Kila mtu aliogopa sana.




Nbukadreza na jeshi lake walizingira Yerusalemu na akachukua watu 10,000 mateka kwa minyororo mpaka Babeli. Ezekieli naye alichukuliwa. Alikuwa na umri wa miaka 25. Wafungwa walichukuliwa kwenda kuishi karibu na Mto wa Kebari iliyo kaskazini mwa Babeli.

Ezekieli aliishi pamoja na Wayahudi lakini yeye na mkewe waliishi kwa nyumba yao. Mwanzoni Wayahudi walilazimishwa na Wababeli kufanya kazi kama watumwa. Maisha yao yalikuwa magumu. Walitamani wawe kwa nchi yao.

Ezekieli alikuwa na uchungu wa kipekee. Alitoka kwa familia ya makuhani. Alitazamia kufanya kazi kwa Hekalu ya Mungu kule Yerusalemu. Alitazamia kuanza kazi ya ukuhani atakapofika umri wa miaka 30. Lakini sasa hangekuwa kuhani akiwa Babeli. Ezekieli alikuwa na uchungu kwa sababu hangeweza kumtumikia Mungu kama kuhani.

Ilifika wakati Ezekieli alikuwa na umri wa miaka 30. Huo ndio umri angeanza kazi ya ukuhani Yerusalemu. Wakati huo huo, Mungu alimwita ili awe nabii kule Babeli. Ezekieli aliona maono ya ajabu ya utukufu wa Mungu. Hayo maono yalikuja kwa kisulisuli.



Kulikuwa na mwangaza mkuu, mawingu ya dhoruba, umeme na moto. Maono yenye Ezekieli aliona ilitosha kumthibidishia nguvu za Mungu na kusudi lake. Mungu alikuwa bado na watu wake hata kama walikuwa watumwa kwa nchi ingine. Mungu aliendelea na kuzudi yake kwa watu wake.

Mungu alisema kwamba alikuwa amemchagua kuwa nabii wa Wayahudi waliokuwa watumwa Babeli. Nabii alipea watu ujumbe wa Mungu. Mara kwa mara ujumbe wa Mungu uliambia watu yatakayokuweco baadaye. Mungu alimwambia Ezekieli kwamba atakuwa na kazi ngumu kama nabii. Wayahudi hawatataka kusikia ujumbe wa Mungu. Lakini lazima Ezekieli awambie maneno ya Mungu, wapende wasipende.

Kulikuwa na manabii wengi wa uongo wakati huo. Waliambia watu uongo. Walijifanya wanasema maneno ya Mungu lakini walisema uongo tu. Ilikuwa vigumu sana watu kujua nani ndiye alikuwa nabii wa kweli. Tena ilikuwa vigumu kujua ujumbe wa kweli uliotoka kwa mungu.

Mungu alimfanya Ezekieli kuwa bubu. Hangeweza kuzungumza. Lakini ujumbe wa Mungu ulipomkujia Ezekieli, Mungu alimfungua kinywa chake ili anene. Ezekieli alizungumza tu wakati Mungu alimpa ujumbe aambie watu. Kwa namna hii, watu walijua kwamba alizungumza maneno ya kweli na ulikuwa ujumbe kutoka kwa Mungu.

Wayahudi waliokuwa Babeli walitaka kurudi kwa nchi yao. Manabii wa uongo waliwahakikishia kwamba hivi karibuni watarudi Israeli. Lakini Ezekieli aliwambia ukweli kutoka kwa Mungu. Ezekieli aliwambia kwamba Mungu alikuwa anawaadhibu kwa sababu walikuwa waovu kwa kuaabudu miungu wengine.

Ezekieli alitenda ishara nyingi na kuwapa jumbe nyingi kutoka kwa Mungu. Aliambia Mfalme Nebukadreza kwamba ataenda kushambulia Yerusalemu tena. Yerusalemu na Hekalu ya Mungu itaharibiwa na watu wengi watapelekwa Babeli kama watumwa. Mungu alisema watakuwa watumwa huko Babeli kwa miaka 70. Halafu watarudi. Ezekieli aliwambia kukubali ujumbe wa Mungu na watuliye Babeli. Aliwambia wajenge nyumba na wapande mashamba kwa sababu watakuwa Babeli kwa muda mrefu.

Watu wengi hawakutaka kukubali ujumbe wa Ezekieli uliotoka kwa Mungu. Ezekieli alikuwa na wakati mgumu kunena na watu wenye hawakutaka kusikiliza.

Siku moja mjumbe alitoka Yerusalemu na habari kwamba Yerusalemu na Hekalu ya Mungu vilikuwa vimeharibiwa. Kutoka wakati huo, Ezekieli hakuwa bubu tena. Alikuwa ameambia watu ujumbe wa ukweli wa Mungu.

Mungu aliadhibu watu wake kwa sababu ya uovu wao. Waliishi Babeli kama watumwa. Lakini kama kawaida Mungu aliwapa watu wake ujumbe wa tumaini. Ezekieli aliwapa unabii mwingi wa ajabu wa tumaini la baadaye. Popote walipo watu wa Mungu, Mungu ako na anawalinda.